# SHULE YA KITAIFA, MARANDA

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)**

## MTIHANI WA MWIGO, 2025

**102/2** **KISWAHILI (Lugha)** **Karatasi ya 2**

**Mei/Juni, 2025** **Muda: Saa 2½**

Jina: …………………………………………….……..…… Nambari: ………...……

Mkondo: ……………….. Sahihi: ……….......... **Jumatatu, 26/5/2025; Saa Nane Alasiri**

**Maagizo**

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Andika mkondo wa kidato chako, tarehe kisha utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali* ***yote.***
d) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
e) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
f) ***Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**1. UFAHAMU** **(Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Ulikuwa wakati wa jioni jua limepunguza udhia wake na *upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu* mfano wa pamba. Kama ilivyokuwa desturi yetu pale chuoni, siku hiyo tuliketi karibu na lango kuu la chuo ili kutafiti kazi mradi tuliyokuwa tumepewa darasani. Sehemu hii tuliipenda sana kwa kuwa kuuchakura mtandao ilikuwa ni bure, bora tu ufahamu nywila ya mtandao huo. Mandhari ya sehemu hii pia yaliwavutia wanafunzi wengi katika sehemu hii.

Tulipotia fahamu, tulipata mazoea haya yamekita mizizi nasi tukawa hatuna budi kuyakumbatia. Hatukuyakumbatia tu, bali tuliyakumbatia kwa dhati ya moyo. Vikao hivi havikuwa tu hazina kubwa kwetu bali pia vilikuwa vya thamani isiyomithilika. Hapa ndipo *tulinoleana bongo* kwa kupashana habari. Leo hii tumo katika mjadala kuhusu kuhusu mfumo mpya wa elimu CBE tuliopewa darasani kama kazi mradi. Nahodha wa kikundi hiki anampa msemaji wa kwanza nafasi, naye hakusita kushika usukani.

“Nionavyo mimi, mfumo wa CBE unafaa kufutiliwa mbali. Serikali haijajiandaa vilivyo ili kuufanikisha mfumo huu wa elimu. Kwanza, mafunzo waliyopewa walimu ili kuufanikisha mfumo huu kamwe hayatoshi. Nionavyo mimi ni kwamba walimu waliopo ambao idadi yao haitoshi, wanatumia elimu ya mfumo wa 8-4-4 kuufunza ule wa CBE. Itawezekanaje mwalimu apate mafunzo ya wiki moja kisha akawa amefuzu kumwelekeza mwanafunzi? Isitoshe mfumo huu unamhitaji sana mwalimu kutumia teknolojia ya kisasa katika ufunzaji. Usishangae nikikwambia kuwa walimu wengi hawana mafunzo ya kisasa ya kompyuta. Zaidi ya hayo shule nyingi vilevile hazina tarakilishi. Baadhi yazo pia umeme haupo. Baada ya serikali kuahidi kuwapa watoto vipakatalishi, je jiulize, ni wanafunzi wangapi hivi sasa ambao walipata vipakatalishi hivyo? Kando na hayo, wazazi wengi washalalamika kuhusu gharama kubwa ya vifaa ambavyo walimu huwatuma wanafunzi kuvileta shuleni. Huenda ikawa sababu ya wao kusema kuwa ni heri mfumo huo wa CBE ukaachiwa shule za kibinafsi.

Muda huo wote kila mtu pale tulipoketi alikuwa ametulia. Wapo waliotikisa vichwa kukubaliana naye Tetesi na wapo waliotikisa kukataa. Mara kijana mmoja tuliyemwita Harakati alisimama na kuzungumza. Mawazo yake Harakati ni kama yalikuwa ya kumpinga Tetesi .

“Mtazamo wangu mimi ni kuwa mfumo wa CBE haufai kufutiliwa mbali. Itakuwa hasara kubwa kwa washika dau mbalimbali ambao wameekeza katika mfumo huu. Ikumbukwe kwamba imeigharimu serikali pesa nyingi katika kujenga madarasa, kuwafunza walimu pamoja na kuchapisha vitabu vya mfumo huu. Isitoshe kuutupilia mbali mfumo huu itakuwa sawa na kuwapotezea muda wanafunzi wa gredi ya tisa, nane, saba na sita ambao kwa muda huu wote wamekuwa wakisoma mfumo huu.”

“Nakuunga mkono Harakati, alianza Wetu ni Wetu. Kwanza Tetesi awazie tena udhaifu wa mfumo 8-4-4 ndipo awazie hayo. Kila mwanafunzi katika mfumo huu wa CBE ni mshindi. Hakuna kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wajinga na werevu.

Isitoshe, katika mtaala huu mpya, hakuna kurudiarudia madarasa kama ilivyo katika mfumo huo wa awali. Vilevile, mtaala wa CBE utawapa wanafunzi wa Kenya matumaini na fursa ya kuimarisha vipawa na uwezo wao. Ikumbukwe kwamba mtaala huu unasisitiza ukuzaji wa talanta za wanafunzi nchini tofauti na ule wa 8-4-4. Pia, CBE humfunza mwanafunzi masomo ambayo tu yatamfaa maishani mwake. Lugha asili za wanafunzi pia zitakuzwa katika mfumo huu mpya. Hivyo basi serikali haina budi kuufanikisha mtaala huu.

Maneno yake Wetu ni Wetu yalifunikwa ghafla na kelele za kumshangilia na kumsifu kijana huyu. Alipoona bado wanashangilia, aliinua mkono wake wa kushoto juu na kusema, “Basi! Basi wanafunzi wenzangu, sina shaka ujumbe umeshafika.

***Maswali***

a) Bainisha mambo yanayoleta utangamano baina ya wanafunzi chuoni? (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b) Eleza changamoto zinazokumba utekelezaji wa mfumo mpya wa elimu. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

c) Onyesha namna wanafunzi wa chuo kikuu wanavyodhihirisha ukomavu. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

d) “Mfumo wa 8-4-4 unafaa kufutiliwa mbali.” Thibitisha kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

e) “Kila mwanafunzi katika mfumo huu wa CBE ni mshindi.” Thibitisha kulingana na makala haya. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

f) Kauli “upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu, “imetumia tamathali gani ya usemi? (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

g) Eleza maana ya “tulinoleana bongo” kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

## 2. UFUPISHO (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Uchafuzi wa mazingira umeongezeka maradufu katika pembe zote za ulimwengu wetu. Kuna aina nyingi za uchafuzi? Kwanza, kuna uchafuzi wa hali anga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili ni aina ya gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili vilevile baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huuharibifu ukanda huo.

Uchafuzi mwingine ni uchafuzi wa kiajali, uchafuzi huu hutokana bila binadamu kukusudia. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingara yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hayo hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila kujali wala kubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, hufanya mazingira yaonekane machafu.

Sote tunajukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafuzi wa mazingira. Kwanza, kuelimisha na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu kwenye vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Tuhakikishe tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuundwa upya na kutumika tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi kwa njia hii tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udongo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka; kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

a) Dondoa mambo muhimu yanayojitokeza katika aya za kwanza nne. (maneno 75 - 80) (alama 9, utiririko 1)

**Matayarisho**

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

**Jibu**

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

.....................................................................................................

b) Ukirejelea aya ya mwisho, eleza namna za kusuluhisha tatizo la uchafuzi wa mazingira.
(maneno 45 - 50) (alama 6, utiririko 1)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**Jibu**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) Andika neno lenye mpangilio ufuatao wa sauti: (alama 2)

Kikwaruzo ghuna cha meno, irabu ya chini, kizuiwa hafifu cha ufizi, vokali tandazwa ya juu ……………………………………………………………………………………

b) Tenganisha na uonyeshe muundo wa silabi katika neno: **funzo**. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

c) Zitumie mofimu hizi kuunda neno: (alama 2)

mofimu ya unominishaji, mzizi, kiishio, kiambishi cha mazoea

……………………………………………………………………………………………

d) Ukitumia kigezo cha uamilifu, ainisha sentensi: Huenda mgeni afike mapema. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………

e) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

i. Tilia daftari lako <u>jalada</u>. (tumia kitenzi badala ya nomino iliyopigwa mstari)

……………………………………………………………………………………….

ii. Yona atasoma tamthilia. (geuza katika wakati uliopita hali timilifu kanushi)

……………………………………………………………………………………………

iii. Mtu amemfanya mtoto afue nguo. (anza kwa neno matoto bila kurudia kitenzi fanya)

……………………………………………………………………………………………

iv. Ameenda chooni baada ya kuzaa. (tumia tasfida.)

……………………………………………………………………………………………

f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi tofauti ya kistari kifupi. ( - ) (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

g) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Utulivu wao uliwawezesha kuwajibikia majukumu yao.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

h) Changanua kwa kutumia jedwali. (alama 4)

Wewe ukija mapema utanipata nakusubiri afisini.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

i) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 2)

"Njoo hapa umwone farasi nitakayekununulia kesho," Sagilu akaita kwa bashasha.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

j) Tunga sentensi **moja** kutofautisha kati ya **sabuni** na **zabuni**. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

k) Tambulisha dhima za vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ambaye amejeruhiwa atatibiwa ilivyoelekzwa na tabibu wake.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

l) Kwa kutolea mifano, taja matumizi **mawili** ya kiambishi **e**. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

m) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

N + RH + t + kijalizo

…………………………………………………………………………………………………

n) Tambua uamilifu wa neno '**katika**' kwenye sentensi ifuatayo. (alama 2)

Katika hekaheka hizo alisahau kitabu katika nyumba akija shuleni.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

o) Tunga sentensi ukitumia: (alama 2)

i. Nomino ya jamii katika ngeli ya I – ZI

…………………………………………………………………………………………………

ii. Kiunganishi cha kinyume

…………………………………………………………………………………………………

p) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Awali, Sihaba alikuwa amewapikia wanawe Mrima pilau vizuri.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

q) Andika sentensi ifuatayo upya kudhihirisha mazoea. (alama 2)

Wale ambao wanaabudu kwa kweli  hupata baraka nyingi maishani.

…………………………………………………………………………………………………

r) Aliyeumia huambia ugua pole, unapotaka mtu akupishe utamwambia ............................ Anapoapa mtu husema walahi! Na unapotaka kuonyesha mtu dharau unamambia ...................................................... (alama 2)

**4. ISIMUJAMII** **(Alama 10)**

a) ***Soma mazungumzo yafuatayo kisha uyatumie kujibu maswali yafuatayo***

Mtu I: Haya nieleze una shida gani?
Mtu II: (*Anashusha pumzi*.) Mmm…. Nina maumivu ya kifua! Je, ni…na kichomi?
Mtu I: (*Huku akiandika*.) Siwezi kuwa na hakika kwa sasa. Kwanza, nataka kukutuma kwenye maabara halafu ufanyiwe eksirei.
Mtu II: (*Akimkabidhi karatasi*.) Nitadungwa sindano lakini? Afadhali tembe!
Mtu I: Usiwe na hofu, utapona. Vipimo vinaonyesha, benki yako haina kitu….*CD4 count* yako iko chini …. Hii ni *emergency*…. Itabidi tukudunge sindano halafu tukupe vidonge ambavyo utameza $2 \times 3$ kwa siku.
Mtu II: Sawa tu. Asante.

i. Tambua sajili inayorejelewa katika mazungumzo haya. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………..

ii. Huku ukitoa mifano kutoka kifunguni, bainisha sifa **sita** za sajili husika. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

b) Eleza namna muktadha unavyoathiri mitindo ya lugha. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO**